# Mwongozo wako wa kuelewa mfumo wa kurudishwa katika nchi ulikotoka kutoka Afrika Kusini



Scalabrini
Centre of Cape Town

## Mwongozo huu unaeleza:

1. Utaratibu wa kuzuiliwa na kurudishwa katika nchi ulikotoka kutoka Afrika Kusini (kwa sababu za sheria ya wakimbizi au uhamiaji pekee)
2. Unachopaswa kufanya ikiwa (au mtu unayemjua) utazuiliwa ili kurudishwa katika nchi ulikotoka
3. Haki zako ni zipi katika utaratibu wa kuzuiliwa na kurudishwa katika nchi ulikotoka

**Nipakue!**

Mwongozo huu una habari na maelezo muhimu ya mawasiliano. Uhifadhi kwenye simu yako na umtumie mtu unayemwamini sasa, anayeweza kukusaidia ikiwa utazuiliwa.

**Muhimu!**

Ikiwa utazuiliwa, tunapendekeza zaidi utafute msaada wa kisheria. Utapata mashirika yanayoweza kukupa habari zaidi hapa.

Mashirika yanayoweza kusaidia

# Yaliyomo

Tunapendekeza usome mwongozo huu kuanzia mwanzo hadi mwisho, lakini unaweza pia kubofya mada zifuatazo ili 'uruke' hadi mahali zilipo katika mwongozo huu.

**Haki zako ukiwa kizuizini**

## Utaratibu wa kurudishwa katika nchi ulikotoka

Katika mwongozo huu, tutaangalia kila hatua ya utaratibu wa kurudishwa katika nchini ulikotoka. Tumegawa utaratibu huu katika hatua nne, lakini unaweza kutofautiana kulingana na hali uliyomo.

1 

**Hatua ya Kwanza**
Kuzuiliwa na polisi au afisa wa uhamiaji

2 

**Hatua ya Pili**
Kupelekwa katika mahakamani

3 

**Hatua ya Tatu**
Ikiwa unafukuzwa nchini, kusafirishwa hadi Lindela

4 

**Hatua ya Nne**
Kurudishwa katika nchi ulikotoka

**Kupanga kurudi katika nchi ulikotoka mwenyewe**

**Mashirika yanayoweza kusaidia**

# Haki zako ukiwa kizuizini

Ni muhimu kukumbuka kuwa, nchini Afrika Kusini, kila mtu ana haki akiwa kizuizini. Haijalishi unakotoka au iwapo una stakabadhi au huna - una haki hizi. Ukiwa kizuizini, una haki ya:

- Kujua kwa nini umezuiliwa.
- Kupiga simu. Ikiwa umezuiliwa, unaweza kuomba kutumia simu iliyo katika kituo cha polisi.
- Kuwa na wakili (au Shirika Lisilo la Serikali la Msaada wa Kisheria (Legal Assistance NGO)/Kliniki ya Sheria (Law Clinic), ikiwa huna uwezo wa kulipia huduma za wakili), na kuwa na mkalimani mahakamani.
- Kutendewa kwa heshima (ikijumuisha kupewa malazi / chakula / matibabu yanayofaa).
- Kufahamishwa haki zako na kupewa maelezo kwa lugha unayoelewa.
- Kutembelewa na familia/washauri wa kidini/madaktari wako.
- Kuwekwa kando na washukiwa wa uhalifu.

**Ikiwa haki zako haziheshimiwi, tafuta msaada wa kisheria.**

Mashirika yanayoweza kusaidia

**Kumbuka, beba nakala za stakabadhi zako kila wakati!**



Je, wajua?

Utaratibu wa kurudishwa katika nchi ulikotoka unaweza kuchukua hadi siku 120, kuanzia wakati unakamatwa. Ikiwa hutafukuzwa nchini baada ya kuzuiliwa kwa jumla ya siku 120, una haki ya kuachiliwa.



# Utaratibu wa kurudishwa katika nchi ulikotoka



## Hatua ya kwanza

**Kuzuiliwa na afisa wa uhamiaji au polisi**



Ni polisi au afisa wa uhamiaji pekee ndiye anaweza kukuomba stakabadhi za kuthibitisha kuwa unaishi nchini Afrika Kusini kisheria. Ikiwa ana 'misingi inayofaa' (sababu thabiti) ya kuamini kuwa huishi nchini Afrika Kusini kisheria, anaweza kukuzuilia anapothibitisha hali yako ya kuwa nchini Afrika Kusini, kwa kawaida katika kituo cha polisi.



Anaweza tu kukuzuilia kwa saa 48 anapokuthibitisha, na lazima ufikishwe mahakamani ndani ya saa 48 au siku inayofuata ya kazi ikiwa itakuwa ni wikendi au sikukuu ya umma.



Ikiwa uchunguzi wao utathibitisha kuwa wewe ni 'mgeni asiye halali,' afisa wa uhamiaji anapaswa kukufahamisha, kwa maandishi, kuwa umeshtakiwa kwa kosa la kuwa 'mgeni asiye halali'. Kisha, utafikishwa mahakamani. Kumbuka, hili lazima lifanyike ndani ya saa 48.




Ikiwa hutafikishwa mahakamani ndani ya saa 48, una haki ya kuachiliwa mara moja.

**Chukua hatua sasa!**

**Ni muhimu sana kuchukua hatua na kupata msaada wa kisheria ukiwa katika hatua hii ya utaratibu! Pata maelezo zaidi kwenye hatua inayofuata.**

## Chukua hatua sasa!

Katika hatua hii ya utaratibu wa kurudishwa katika nchi ulikotoka (Hatua ya Kwanza), unapokamatwa mara ya kwanza, ni muhimu kuchukua hatua. Hii inalingana na aina ya stakabadhi ulizo nazo. Hapa chini, tafuta taarifa ambayo ni sahihi kuhusu hali ya stakabadhi zako, na ufuate maelezo ili uelewe unachopaswa kufanya.

### Nina stakabadhi sahihi

(ikijumuisha hali ya ukimbizi, viza ya mtafuta hifadhi ya kimbilio, viza yoyote sahihi ikijumuisha ZEP)

**Jambo la kufanya**

Onyesha afisa nakala yako iliyothibitishwa au viza halisi/kibali/PDF ya viza ya mtandaoni (e-visa)/barua pepe

**Jambo linalofuata**

Lazima uachiliwe - lakini baada tu ya afisa kuthibitisha stakabadhi zako za utambulisho

**Maelezo muhimu**

Asipokuachilia, tafuta msaada wa kisheria. Ikiwa huna stakabadhi zako, uliza afisa ikiwa mtu anaweza kukuletea stakabadhi zako. Ikiwa hatakubali, mwambie kwamba ni lazima athibitishe hali au utambulisho wako ndani ya saa 48. Utaachiliwa baada ya kutoa stakabadhi zako na hali yako kuthibitishwa. Asipokuachilia, tafuta msaada wa kisheria. Angalia ukurasa wa 15 wa mwongozo huu.

## Mimi ni mgeni ninayetafuta hifadhi ya kimbilio, lakini sina stakabadhi

**Jambo la kufanya**

Eleza kuwa umetoroka nchi yako kwa sababu haikuwa salama na unataka kuomba hifadhi ya kimbilio nchini Afrika Kusini.

**Jambo linalofuata**

Katika hatua hii ya utaratibu, unapaswa kuachilia ili uombe hifadhi ya kimbilio, lakini huenda ukazuiliwa wakati Ofisi ya Masuala ya Nyumbani (Home Affairs) inakusaidia kuomba hifadhi katika Ofisi ya Kupokea Wakimbizi (Refugee Reception Office).

**Maelezo muhimu**

Unapaswa kupata msaada wa kisheria. Unaweza kuwasiliana na shirika kwa kubofya hapa.

Mashirika yanayoweza kusaidia

## Nina viza au kibali ambacho muda wake wa matumizi umeisha

**Jambo la kufanya**

Muonyeshe afisa viza/kibali chako cha mtafuta hifadhi ya kimbilio, hali ya ukimbizi au viza ambayo muda wake wa kutumika umeisha na ueleze kwa nini muda wake wa kutumika umeisha.

**Jambo linalofuata**

Katika hatua hii ya utaratibu, huenda ukazuiliwa. Huenda ukapigwa faini au kufungwa jela. Msaada wa kisheria usiolipishwa unapatikana mahakamani ili kukusaidia ikiwa utashtakiwa kwa kuwa na stakabadhi ya mkimbizi au viza/kibali cha mtafuta hifadhi ya kimbilio ambacho muda wake wa kutumika umeisha.

## Sina stakabadhi zozote za kisheria. Sina stakabadhi.

**Jambo la kufanya** — Mweleze afisa kwa nini huna stakabadhi nchini Afrika Kusini.

**Jambo linalofuata** — Katika hatua hii ya utaratibu, huenda ukazuiliwa au kuachiliwa chini ya hali fulani. Pata msaada wa kisheria.

**Maelezo muhimu** — Unapaswa kupata msaada wa kisheria. Unaweza kuwasiliana na shirika kwa kubofya hapa.

Mashirika yanayoweza kusaidia

## Niliomba hifadhi ya kimbilio, lakini ombi langu limekataliwa

**Jambo la kufanya** — Unapaswa kuomba upewe muda wa kutosha ili ujiandae kuondoka nchini.

**Jambo linalofuata** — Unapaswa kupewa ‘amri ya kuondoka’, na muda ambao unahitaji kuondoka Afrika Kusini.

**Dokezo muhimu** — Ikiwa hutapewa ‘amri ya kuondoka’ na umezuiliwa, wasiliana na mashirika ya kisheria mara moja!

## Tofauti kati ya kizuizi cha kiusimamizi na cha uhalifu

Katika Hatua ya 1 ya utaratibu wa kuzuiliwa, ikiwa afisa wa uhamiaji anaamini kuwa uko nchini Afrika Kusini "kinyume cha sheria", anapaswa kukupa fomu inayosema hivi. Kwenye karatasi hiyo, itasema Kifungu cha sheria ya Uhamiaji unachoshtakiwa chini yake. Section 34 ni kizuizi cha "kiusimamizi" cha kurudishwa katika nchi ulikotoka. Section 49 ni kizuizi cha "uhalifu" na si cha kurudishwa katika nchi ulikotoka. Tofauti kati ya aina hizi za vizuizi zimeelezwa hapa chini:

**Kizuizi cha uhalifu**

Kizuizi cha uhalifu hufanyika unaposhtakiwa kwa kosa, ikijumuisha kosa la kuingia au kuishi nchini kinyume cha sheria. (Hii ni chini ya Section 49 of the Immigration Act.) Kwa suala lolote la uhalifu, ikiwa huwezi kulipia huduma za wakili, una haki ya kupata msaada wa kisheria bila kulipishwa.

Ikiwa utashtakiwa chini ya Section 49 of the Immigration Act na upatikane na hatia, lazima kwanza ufungwe jela (kwa kipindi cha miaka 2 hadi 4) au ulipe faini kabla ya uwezekano wa kurudishwa katika nchi ulikotoka. Hata baada ya hayo, bado huenda ukazuiliwa au kukamatwa tena ili kurudishwa katika nchi ulikotoka chini ya Section 34. Siku 120 za kuzuiliwa zitaanza mara tu unapokamatwa au kuzuiliwa ili kurudishwa katika nchi ulikotoka. Tafuta msaada wa kisheria mara moja.

---


**Kizuizi cha Kiusimamizi**

Kizuizi cha kiusimamizi hufanyika wakati unazuiliwa ili kurudishwa katika nchi ulikotoka baada ya kupatikana kuwa "mgeni asiye halali." (Hii ni chini ya Section 34 of the Immigration Act.) Ikiwa umezuiliwa chini ya kifungu hiki, lazima ufikishwe mbele ya hakimu ambaye ataamua ikiwa unapaswa kuachiliwa au kurudishwa katika nchi ulikotoka.




**Kwenye ukurasa unaofuata, utaona Hatua ya 2 ya utaratibu wa kuzuiliwa kwa wanaozuiliwa kwa makusudi ya kiusimamizi.**

Rudi kwenye ukurasa wa yaliyomo




# Hatua ya Pili

## Kufikishwa mahakamani



Polisi atakupeleka katika jela za mahakama kabla ya kufikishwa mahakamani. Hakimu ataamua ikiwa wewe ni raia wa kigeni na, ikiwa hivyo, iwapo una sababu sahihi ya kuwa nchini.



Mahakamani, ni muhimu uwe na msaada wa kisheria. Una haki ya kuwa na wakili au kuomba msaada wa kisheria. Mahakamani, lazima ueleze hali ya stakabadhi zako kwa wakili wako na hakimu (jaji). Kuwa mwaminifu na utoe maelezo mengine iwezekanavyo. Ikiwa hakimu anaamini kuwa una sababu nzuri ya kuwa nchini Afrika Kusini, basi ata:

- amrishwa uachiliwe au,
- amrisha uachiliwe na kuagiza idara ya Masuala ya Nyumbani (Home Affairs) ikusaidie kupata stakabadhi.



Ikiwa sababu zako nzuri za kuwa nchini Afrika Kusini hazieleweki, mahakama inaweza kuruhusu idara ya Masuala ya Nyumbani (Home Affairs) kufanya uchunguzi zaidi na, ikithibitishwa, itaamrisha kuzuiliwa kwako hadi utakapoomba hifadhi kirasmi. Unaweza kuendelea kuzuiliwa hadi utakaporudishwa mahakamani.



Ikiwa hakimu anaamini kuwa huna sababu nzuri ya kuwa nchini Afrika Kusini, basi ata:

- ongeza muda wako wa kuzuiliwa ili kurudishwa katika nchi ulikotoka, kukubaliana na idara ya Masuala ya Nyumbani (Home Affairs) au
- kukuachilia ili ushughulikiwe jinsi ya kurudishwa katika nchi ulikotoka bila kuzuiliwa, chini ya hali fulani.

Ikiwa jaji atakubali kuwa unapaswa kushtakiwa kulingana na Section 49, hii inajulikana kama kuzuizi cha uhalifu (si cha kiusimamizi). Ikiwa utapatikana na hatia utalazimika kufungwa jela au kulipa faini kabla ya kurudishwa katika nchi ulikotoka au kupata stakabadhi nchini Afrika Kusini. Ikiwa si salama kwako kurudi katika nchi yako, unapaswa kupinga kuzuiliwa. Tafadhali tafuta msaada wa kisheria usiolipishwa.

Rudi kwenye ukurasa wa yaliyomo

3 

# Hatua ya Tatu

## Kusafirishwa hadi Lindela



Ikiwa unapaswa kurudishwa katika nchi ulikotoka, utazuiliwa katika kituo cha polisi.



Kwa kawaida, utasubiri hadi upelekwe katika Lindela Repatriation Centre, karibu na Johannesburg. Wakati mwingine mtu hurudishwa katika nchini alikotoka akiwa katika kituo cha polisi bila kupelekwa katika kituo cha Lindela, lakini kwa kawaida huwa hivyo tu ikiwa unarudishwa katika nchi jirani.




Ikiwa utazuiliwa zaidi ya siku 120, una haki ya kuachiliwa.



Lindela Repatriation Centre ni kituo kikubwa zaidi nchini Afrika Kusini cha kuwarudisha watu katika nchi yao. Kiko karibu na Johannesburg.

Rudi kwenye ukurasa wa yaliyomo

4



# Hatua ya Nne

## Kurudishwa katika nchi ulikotoka



Idara ya Masuala ya Nyumbani (Home Affairs) itapanga utakavyorudishwa katika nchi ulikotoka. Una haki ya kujua kinachoendelea; wakati na jinsi utakavyorudishwa katika nchi ulikotoka.



Unaweza kurudishwa katika nchi ulikotoka kwa basi au ndege. Kumbuka, Ikiwa utazuiliwa zaidi ya siku 120, una haki ya kuachiliwa.



Baada ya kurudishwa katika nchi ulikotoka, kuna uwezekano utatangazwa kuwa ‘hufai’ (umepigwa marufu kurudi tena Afrika Kusini) hadi miaka mitano, na hii inaweza kuathiri maombi yako ya viza ya baadaye, hata baada ya marufuku yako kuondolewa.



Rudi kwenye ukurasa wa yaliyomo

# Kupanga kurudi katika nchi ulikotoka mwenyewe

Wakati mwingine, unaweza kupanga kurudi katika nchi ulikotoka mwenyewe.

Wakati mwingine, unaweza kupanga kuondoka Afrika Kusini mwenyewe ikiwa unaweza:

- Kuonyesha stakabadhi sahihi ya usafiri
- Kununua tiketi ya ndege (kwa kawaida ya ndege ya moja kwa moja) ya kwenda katika nchi ulikotoka

Ikiidhinishwa, utakaa kizuizini hadi tarehe ya safari yako ya ndege na kupelekwa katika uwanja wa ndege na afisa wa uhamiaji. Familia au marafiki zako wanapaswa kuhakikisha kuwa vitu vyako viko katika uwanja wa ndege ili uweze kusafiri. Ikiwa unaweza kupanga safari yako mwenyewe ya kurudi katika nchi yako, tunapendekeza zaidi ufanye hivyo - mradi ni salama kwako kurudi katika nchi yako. Kupanga safari yako mwenyewe ya kurudi katika nchi ulikotoka mara nyingi kunaweza kufupisha muda wako wa kuzuiliwa.

**Kumbuka!**

**Watu wanaotafuta hifadhi (iwe wana stakabadhi au hawana) na wakimbizi hawawezi kurudishwa katika nchi walikotoka na wanalindwa na kanuni ya kutolazimishwa kurudi katika nchi walikotoka. Huwezi kurudishwa katika nchi ambako maisha, uhuru au haki zako zitakuwa hatarini.**





Rudi kwenye ukurasa wa yaliyomo

# Mashirika yanayoweza kusaidia

Ikiwa utakamatwa au kuzuiliwa kwa makusudi ya kurudishwa katika nchi ulikotoka, tunapendekeza zaidi utafute msaada wa kisheria. Una haki, ukiwa kizuizini, ya kutembelewa na mwenzi au familia na washauri wa kidini wanaoweza kukusidia katika kutafuta msaada wa kisheria. Ikiwa utakamatwa ili kurudishwa katika nchi ulikotoka na huna uwezo wa kulipa gharama ya wakili, unapaswa pia kuwasiliana na shirika lisilo la faida lililotajwa hapa chini.

**National Immigration Detention Hotline**

081 716 8791

0800 079 614 (bila kulipishwa )

**Lawyers for Human Rights (Durban)**

031 301 0531

**Nelson Mandela University Refugee Rights Centre (Gqeberha)**

041 504 1310 or 041 504 4705

**University of Cape Town Refugee Rights Clinic (Cape Town)**

021 650 5581

078 594 5591

**Scalabrini Centre of Cape Town**

021 465 6433

078 260 3536

Rudi kwenye ukurasa wa yaliyomo



Funded by the European Union

Contracted by

This document was produced with the financial assistance of the European Union, contracted by ICPMD through the MMD Grant Facility. The contents of this document are the sole responsibility of the Scalabrini Centre and can under no circumstances be regarded as reflecting the position of the European Union or ICMPD.